**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# MWONGOZO WA URATIBU WA WAJANE TANZANIA

**JUNE, 2025**

## DIBAJI

Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingi zinazoendelea inatambua Wajane kama kundi kubwa na nguzo muhimu katika kuchochea ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi jumuishi ili kupata maendeleo endelevu ya watu na Taifa kwa ujumla. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Wajane wana jukumu kubwa la kulea familia kwa kujihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuweza kumudu kupata mahitaji ya lazima ya familia zao na wanachangia kwa kiasi kikubwa kuinua uchumi wa nchi na kupunguza ukosefu wa ajira.

Pamoja na mchango mkubwa wa shughuli za Wajane, zipo changamoto mbalimbali zinazoathiri kundi hili. Baadhi ya changamoto hizo ni kama kuachwa katika hali ya msongo wa mawazo kutokana na kuondokewa na mwenza ambaye kwa wengi wao ndio nguzo ya familia katika pato la kaya na familia. Hali hii hupelekea wajane wengi kushindwa kumudu maisha kutokana na umaskini, kunyimwa haki ya kurithi na kumiliki ardhi na mali. Pia zipo baadhi ya mila na desturi kandamizi kama vile za kurithiwa baada ya kufiwa na wenza, kufukuzwa nyumbani mwao na ndugu wa wenza wao pamoja na kutengwa au kunyanyaswa. Vilevile, wajane hukumbana na changamoto za ukosefu wa mitaji, matumizi ya teknolojia duni katika shughuli za uzalishaji mali, ukosefu wa huduma za ushauri, pamoja na mfumo dhaifu/hafifu wa uratibu na usimamizi wa haki za Wajane.

Kuandaliwa kwa Mwongozo huu ni hatua muhimu katika kutekeleza adhma ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kuwa haki na ustawi wa makundi maalum katika jamii wakiwemo Wajane inapatikana. Mwongozo huu unalenga kujenga uelewa wa pamoja wa namna ambavyo kundi hili linaweza kuratibiwa vyema. Matokeo ya utekelezaji wa Mwongozo huu ni kuweka mifumo endelevu itakayowezesha kupata taarifa za wajane na utatuzi wa changamoto zinazowakabili katika Ustawi na Maendeleo ya familia zao na Taifa kwa ujumla.

Natoa wito kwa Wadau wote wanaohusika na kundi hili kutumia Mwongozo huu ili kufikia adhma ya Serikali ya kuwa na ustawi wa familia.



Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)
**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**YALIYOMO**

DIBAJI

YALIYOMO ..... ii

VIPUPISHO VYA MANENO ..... iv

TAFSIRI YA MANENO ..... v

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..... 1

1.0 Usuli ..... 1

1.1 Hali Halisi Ya Wajane ..... 3

1.2 Malengo ya Mwongozo ........................................................6
1.2.1 Lengo kuu .......................................................................6
1.2.2 Malengo Mahsusi ..............................................................6
1.3 Umuhimu wa mwongozo......................................................7
1.4 Walengwa wa Mwongozo ....................................................8
SURA YA PILI ........................................................................9
2.0 Huduma Kwa Wajane .........................................................9
2.1.1 Msaada wa kisheria .........................................................9
2.1.2 Huduma ya msaada wa kisaikolojia.................................10
2.1.3 Kuunganishwa na fursa mbalimbali ................................11
SURA YA TATU: ...................................................................11
3.1 Uratibu kwa Wajane..........................................................11
3.2 Shirikisho la Wajane .........................................................13
3.3 Uteuzi wa Mratibu wa Wajane ...........................................13
3.4 Majukumu ya Mratibu.........................................................14
SURA YA NNE: MAJUKUMU YA WADAU ...............................15
4.1 Wajibu na Majukumu ya Wadau .........................................15
4.3 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ..........................................................................16
4.4 Ofisi ya Rais TAMISEMI .....................................................17
4.5 Wizara ya Fedha................................................................18
4.6 Wizara ya Katiba na Sheria ...............................................19

4.7 Tawala za Mikoa ........................................................................20
4.8 Mamlaka za Serikali za Mitaa .............................................20
4.9 Ofisi ya Kata..........................................................................22
4.10 Ofisi ya Mtaa/ Kijiji..............................................................23
4.11 Asasi za Kiraia ....................................................................24
4.12 Viongozi wa dini ..................................................................24
4.13 Wajane..................................................................................26
SURA YA TANO: UFUATILIAJI NA TATHMINI .........................26
5.1. Ufuatiliaji ..............................................................................27
5.2. Tathmini ...............................................................................28
6.0 HITIMISHO ...........................................................................31
ORODHA YA MAANDIKO YALIYOTUMIKA.............................32

## VIPUPISHO VYA MANENO

AZAKI Asasi za Kiraia

CCWWT Chama Cha Wajane Tanzania

Convention for Elimination of All Forms of

CEDAW

Discrimination Against Women

Cooperative Rural Development Bank (Benki ya

CRDB

Maendeleo ya Ushirika Vijijini)

MTAKUW Mpangokazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya

WA wanawake na Watoto

MTEF Medium-Term Expenditure Framework

National Bank of Commerce (Benki ya Taifa ya

NBC

Biashara)

NMB National Microfinance Bank (NMB)

OR –

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

TAMISEMI

PPRA Public Procurement Regulatory Authority

TAWIA Tanzania Widow Association

Tanzania Commercial Bank (Benki ya Biashara

TCB

Tanzania)

UWAKI Ukatili wa Kijinsia

WDF Women Development Fund

WMJJWM Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na

M Makundi Maalum

**TAFSIRI YA MANENO**

| | |
|---|---|
| **Afua** | Shughuli mbalimbali zinazotekelezwa katika jamii kwa lengo la kuleta afueni kwa kundi au jumuiya. |

Kitendo cha mwanamke mjane kushiriki tendo la ndoa na ndugu wa marehemu mume wake bila **Mila ya** ridhaa yake (kaka au mdogo wa marehemu)

**Kutakasa** kwa imani ya kuwa ni kuondoa mkosi na laana katika familia na ukoo.

**Mjane** Mwanamke aliyefiwa na mwenza wake na hajaolewa tena na ikathibitika kuwa alikuwa na ndoa ya kimila/ kidini/ kiserikali au waliishi kwa miaka miwili mfululizo na jamii ikathibitisha pasipo na mashaka kuwa wao ni mke na mume kisheria na ujane hufikia ukomo wake pindi tu anapoolewa tena

**Mtoa huduma ya msaada wa kisheria** Ni mtu au taasisi inayotoa usaidizi wa kisheria kwa watu au makundi ya watu ambao hawawezi kumudu gharama za wanasheria au wanahitaji msaada katika kuelewa na kutekeleza haki zao za kisheria. Huduma hii inaweza kutolewa na wanasheria waliobobea, mawakili wa umma, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), au hata watu waliofunzwa kisheria lakini wasio wanasheria wa kitaaluma.

**Ukatili wa Kijinsia** Kitendo chochote anachofanyiwa mwanamke au mwanaume chenye kuleta madhara ya kimwili,, kisaikolojia, kiuchumi au kiakili.

**Wadau** Wizara, Taasisi za Umma, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Sekta binafsi, Jamii, watu binafsi ambao watatekeleza Mwongozo huu na Wajane.

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.0 Usuli

Wajane ni kati ya kundi kubwa la wanawake walioko nchini Tanzania ambao ni zaidi ya asilimia 51 kulingana na Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Kundi hili la wajane lina wanawake wengi wakiwemo vijana na wazee. Wajane katika Mataifa mbalimbali hutambulika kuwa ni kundi maalum kutokana na kukabiliwa na changamoto za kipekee ikilinganishwa na makundi mengine ikiwemo kuondokewa na wenza wao. Umoja wa Mataifa kwa kuliona hilo ulipitisha Azimio Maalum Namba A/RES/65/189 la Disemba 2010 ambalo lilitambua na kuanzisha Siku maalum ya Wajane Duniani inayoadhimishwa Juni 23 ya kila mwaka. Aidha, kuna Mikataba, Maazimio na Mipango ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa inayotoa msukumo wa kushughulikia masuala ya Wajane kipekee ambayo ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW 1979); Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (1989) ambao unalenga katika haki mahsusi za Mtoto; Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (1948); Mkataba wa Afrika wa Haki za Watu na Binadamu (1981); Azimio la Ulingo wa Beijing (1995); Ajenda ya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Ajenda ya Maendeleo ya Bara la Afrika 2063; na Azimio la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) la Jinsia na Nyongeza yake ya Kuzuia na Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (1997) na Mkataba wa Maputo unaosisitiza haki za wanawake wa Afrika.

Kulingana na utafiti uliofanywa na Umoja wa Mataifa unabainisha kuwa wajane ni kati ya asilimia 7 hadi 16 ya wanawake wote duniani, ambapo inakadiriwa kuwa wajane duniani ni takribani millioni 258, kati ya hao wajane millioni 115 wanaishi kwenye umasikini uliokithiri, huku wengi wao wakikabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile kudhulumiwa mali, kufanyiwa ukatili, kutengwa na jamii na kutothaminiwa ndani ya familia na jamii. Kwa Tanzania, matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, inaonesha kuwa idadi ya wajane ni asilimia 4.4 ya wanawake wote nchini ambao jumla yao ni Milioni 31,687,990. Mikoa yenye wajane wengi ni pamoja na Dar es Salaam wenye wajane 103,771 ukifuatiwa na Dodoma (85,669); na Mbeya (82,714). Mkoa wenye wajane wachache ni Katavi ambao idadi yao ni 17,598.

Serikali katika kulinda haki za Wajane, inatekeleza jitihada mbalimbali za kuendeleza wajane ambazo ni pamoja na uwepo wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum iliyoundwa mwaka 2022, ikiwa ni dhamira ya dhati ya Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kushughulikia changamoto za Wajane na wanawake kwa ujumla. Vilevile, Serikali imehuisha Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023), Kuandaliwa kwa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 ambayo inatoa usaidizi wa kisheria kwa

makundi maalum ikiwemo Wajane. Pia kuundwa kwa vyama vya wajane Tanzania kama vile Chama Cha Wajane Tanzania

(TAWIA), Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT) Amazing Grace Africa ambavyo vimechangia katika kuunganisha wajane nchini. Jitihada hizo zimelenga kukuza ustawi wa Wajane.

Pamoja na jitihada zilizopo, wajane bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na kuachwa katika umaskini baada ya wenza wao kufariki, kunyimwa haki ya kurithi na kumiliki ardhi na mali, kufukuzwa kwenye makazi yao na ndugu wa wenza wao, kutengwa na kunyanyaswa. Aidha, Watoto wao mara nyingi hujikuta wameathirika kwa kukosa mahitaji muhimu na kupelekea kuondolewa shuleni na wako katika hatari zaidi ya unyanyasaji na kufanyiwa vitendo vya ukatili hasa wasichana. Kuna tafiti mbalimbali zinazoonesha kuna baadhi ya wajane ambao ni wazee wenye kulemewa na ulezi wa familia zao (HelpAge International 2021); pia wajane ambao wana umri mdogo wanakumbana na changamoto ya kurithiwa na kunyanganywa mali (Mhoja 2008).

### 1.1 Hali Halisi Ya Wajane

Wajane ni moja ya kundi ambalo wengi wao wako katika umasikini uliokithiri kwa sababu wengi wao hunyang’anywa mali zao zinazoondosheka na zisizoondosheka na kuondolewa haki yao ya kujiamulia juu ya mustakabali wa maisha yao baada ya kuondokewa

na wenza wao, kadhalika kufanyiwa ukatili unaowaathiri kimwili, kiuchumi na kisaikolojia. Wengi wao wanakuwa katika mazingira duni na hawawezi kukidhi kujihudumia katika maisha yao, kwa mfano matibabu na lishe ya kila siku ya watoto wao. Ni kundi maalum ambapo Serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuwahudumia. Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 inaonyesha kuwa, Tanzania ina jumla ya wajane **1,396,262** nchini ambapo Mikoa inayoongoza kwa wingi wao ni pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam wenye wajane **103,771** ukifuatiwa na Dodoma **85,669** na Mbeya **82,714**. Mkoa wenye wajane wachache ni Katavi ambao idadi yao ni **17,598**.

Wajane katika Mikoa mbalimbali ya Tanzania wanakabiliwa na changamoto ambazo ni vikwazo kwa maendeleo yao. Miongoni mwa changamoto hizo ni uwepo wa baadhi ya sheria za kimila zinazobagua wajane ikiwemo Sheria ya Kimila ya Mirathi (1963) na sheria mbali mbali za kidini, ambayo imetoa mgawanyo wa mali za marehemu kwa madaraja huku ikimuacha mjane na watoto wa kike katika nafasi ya kupata kiwango kidogo cha mali iliyoachwa ikiwa ni pamoja na kuruhusu kutumia ardhi pasipo kuimiliki. Katika makabila tofauti kuna mila ambazo ni kandamizi kwa wajane ikiwa ni pamoja na mila ya kutakasa mjane ambayo mwanamke mjane hulazimika kuingiliwa kimwili kwa maelezo ya kuwa ni kuondoa mkosi katika familia/ukoo, wajane kurithiwa kuolewa na shemeji yake (kaka/mdogo wa marehemu au binamu pasipo ridhaa). Mila hizi zimepelekea wajane wengine kupata magonjwa na hata ulemavu

(Mhoja 2008). Vilevile, Wajane wameendelea kukosa huduma nzuri na stahiki kutokana na sababu mbalimbali. Mathalani mjane katika baadhi ya jamii anapofiwa na mwenza wake hatakiwi kuolewa, badala yake hutakiwa kuendelea kubaki kwenye familia na kulea watoto hadi hapo watoto watakapokuwa wakubwa na kuweza kujitegemea (Agarwala 1963; Mhoja 1995). Jambo hili huwafanya wajane kuwa wategemezi wa watoto wao wa kiume (Vlassoff 1990; Mhoja 1997). Aidha, jamii nyingine huwachukulia wajane kuwa ni watu wabaya ambao wamewaua waume zao (Jarida la umoja wa Wanawake 1990; Mhoja 2008). Hii husababisha wajane wengi kukimbia miji yao na kwenda maeneo mengine ya mijini ili kutafuta usalama wa kuishi kwa kuwa kwenye vijiji vyao hawahitajiki na wanafukuzwa kama wauaji. Kimsingi, Mazingira kama haya yanadhihirisha kuwa ujane si hali nzuri na huwakosesha amani na furaha wajane wengi Duniani, Vilevile huleta msongo wa mawazo na magonjwa ya Sonona kwa wajane. Hali hii hupelekea kutoshiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali na kubaki katika lindi la umaskini. Unyanyasaji huu umepelekea hata wajane wengine kupoteza Maisha (Mhoja 2008).

Kutokana na mazingira kama haya, wajane hujikuta wanakabiliwa na changamoto ya kukosa uhuru wa kujieleza na kujiamulia mambo yanayoathiri mustakabali wao na kunyimwa haki ya kumiliki mali na ardhi. Hii inachangiwa na wajane kutokuwa na uelewa na ufahamu wa haki zao, hivyo hupelekea wengi wao kunyang'anywa mali

waliyochuma na wenza wao na kubaki wakihangaika na watoto wao pamoja na familia zao kwa ujumla.

Kwa kutambua changamoto za wajane, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum yenye dhamana na makundi maalum imeandaa mwongozo mahsusi wa uratibu wa wajane ili kuongeza kasi na juhudi za Serikali na wadau katika kushughulikia changamoto za wajane na maendeleo yao nchini.

## 1.2 Malengo ya Mwongozo

### 1.2.1 Lengo kuu

Kuimarisha uratibu wa wajane ili kuwa na mfumo imara kwa ustawi na maendeleo ya wajane nchini

### 1.2.2 Malengo Mahsusi

i. Kuainisha taratibu za uratibu na usimamizi wa masuala ya wajane nchini;

ii. Kuwezesha ngazi za msingi (Mtaa/kijiji) kuwa na utaratibu wa kubaini na kuchambua taarifa za wajane ikiwa pamoja na kushughulikia changamoto zao;

iii. Kuanisha muundo wa utekelezaji na majukumu ya kila mdau katika utekelezaji na uendeshaji wa afua za Wajane;

iv. Kuainisha mipaka ya kiutendaji ya ngazi za msingi na wadau wengine katika kushughulikia masuala ya wajane;

v. Kuimarisha mawasiliano kati ya Wizara yenye dhamana, Wizara za Kisekta, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na uongozi wa wajane;

vi. Kusaidia uwepo wa mazingira wezeshi/saidizi ya kimfumo kuanzia ngazi ya familia itakayo changia kupungua kwa ongezeko la umaskini kwa wajane.

vii. Kujenga misingi saidizi itakayosaidia kupunguza kiwango cha uhanga wa ujane kwa wajane kuanzia mjane mmoja mmoja.

viii. Kuwezesha jamii kuelewa masuala ya wajane na changamoto zinazowakabili na namna wanaweza kuwasaidia kukabiliana nazo.

## 1.3 Umuhimu wa mwongozo

i. Kukuza uelewa kwa jamii kuhusu wajane na masuala yanayohusu haki na wajibu wao;

ii. Kuimarisha uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa changamoto zao;

iii. Kuwezesha wadau katika ngazi mbalimbali za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi iliyowekwa ili kuboresha hali na ustawi wa wajane nchini.

### 1.4 Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu ni kwa ajili ya wadau wote wanaohusika na masuala ya utu, haki na usawa hususani kwa wajane nchini.

Hivyo, watumiaji wa Mwongozo huu ni pamoja na Wajane wenyewe, Wizara za Kisekta, Asasi za Kiraia (AZAKI), Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo wanaotekeleza afua zinazogusa haki na ustawi wa wajane na jamii ya yote Tanzania bara.

# SURA YA PILI

## 2.0 Huduma Kwa Wajane

Kulingana na changamoto wanazopitia wajane, zilizo nyingi zinatokana na uelewa wao mdogo wa masuala mbalimbali ikiwemo huduma zinazotolewa kwao. Hivyo, sura hii ya Mwongozo inaainisha huduma ambazo ni muhimu kwa Wajane kuzifahamu, kuelewa wanazifikiaje na mazingira ya kutolewa kwake hapa nchini zinazolenga kuboresha hali ya maisha ya wajane kwa kuwapa msaada wa kisheria, kijamii, na kibinadamu. Huduma hizo ambazo hutolewa na Serikali kwa kushirikiana na wadau ni pamoja na:-

### 2.1.1 Msaada wa kisheria

Huduma hizi zinahusisha ushauri kuhusu urithi, mirathi, haki za watoto, na masuala mengine ya kisheria. Wajane wanazo changamoto mbalimbali ambazo huhitaji huduma ya msaada wa kisheria. Masuala ambayo wanawake wamekuwa wakihitaji msaada wa kisheria ni pamoja na masuala ya ardhi, mirathi, kudhulumiwa mali na kunyanyaswa.

Serikali ilipitisha Sheria Na. 1 ya mwaka 2017 ya huduma ya msaada wa Kisheria kwa lengo la kuhakikisha wananchi hususan wa makundi maalum wanapata msaada wa kisheria kwa masuala yanayowakabili. Kupitia sheria hii watoa huduma za msaada wa kisheria wanasajiliwa na kupatikana kuanzia ngazi ya kitongoji. Kumekuwa na uhitaji mkubwa wa wajane kuelewa sheria, hivyo kuna haja ya kuhakikisha wanashiriki kampeni mbali mbali kama Mama

Samia Legal Aid Compaing na elimu mbalimbali zinatolewa katika maeneo yao ili kuelewa sheria mbalimbali kulingana na changamoto zao. Pia Watoa huduma ya msaada wa kisheria waliopo watambulike ikiwa ni pamoja na kufahamika mahali walipo kwa lengo la kuwarahisishia wajane kufahamu mahali pa kufikisha masuala yao ya kisheria.

### 2.1.2 Huduma ya msaada wa kisaikolojia

Huduma za ushauri wa kisaikolojia zinatolewa ili kusaidia wajane kukabiliana na maombolezo na msongo wa mawazo. Huduma hizi hutolewa na wataalamu wa Ustawi wa Jamii, wataalamu wa afya ya akili na wanasaikolojia katika ngazi zote. Ni muhimu elimu itolewe kuhusu huduma hizi kwa wajane kwa kuwa kumekuwepo na masuala mbalimbali ambayo hupelekea wajane kukumbwa na msongo wa mawazo na afya ya akili. Matatizo kama vile kunyanyaswa, kutengwa, kudhulumiwa mali, migogoro ya familia au kunyang'anywa watoto vinavyochangia wajane walio wengi kupoteza muelekeo wa maisha na wengine kuchanganyikiwa. Huduma ya msaada wa kisaikolojia katika ulimwengu wa sasa ni ya muhimu kwa wajane katika kuwanusuru na matatizo waliyonayo ya afya ya akili. Hivyo, wajane kwa kuzingatia mahali walipo wafikiwe na kupatiwa huduma ya msaada wa kisaikolojia kupitia njia mbalimbali zitakazobuniwa. Huduma hii inaweza kutolewa kwa utaratibu kama vile kuwa na kliniki maalum, au mafunzo ya mara kwa mara kwao

pamoja makundi mengine ya kijamii inayolenga kujengana kisaikolojia na kuimarishana.

### 2.1.3 Kuunganishwa na fursa mbalimbali

Huduma hizi zinahusisha Wajane kuunganishwa na fursa mbalimbali zikiwemo majukwaa mbali mbali yanayowaunganisha na kuwa na sauti moja, vikundi mbalimbali vya kiuchumi, programu na afua mbali mbali zinazoanzishwa, kuunganishwa na taasisi za mikopo yenye masharti nafuu na zisizo na riba ili kuwasaidia kuanzisha biashara au kuongeza biashara zilizopo. Mikopo hii mara nyingi inapatikana kupitia taasisi za kifedha za umma au za kibinafsi.

Wajane wahamasishwe kujiunga kwenye vikundi na kujishughulisha na ujasiriamali ili kujiongezea kipato kwani kumekuwa na hali ya wajane kutofaidika na fursa mbalimbali za kiuchumi nchini. Kwa mfano, Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini inatoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake. Hata hivyo, wajane wengi wamekuwa hawajitokezi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kujinyanyapaa wenyewe.

## SURA YA TATU:

### 3.1 Uratibu kwa Wajane

Sehemu hii inaelekeza namna mwongozo utakavyotumika kuratibu huduma kwa wajane kwa kuhakikisha kundi la wajane linahudumiwa kuanzia ngazi ya Mtaa/kijiji hadi Taifa. Wajane wote na wadau wa masuala ya wajane watatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

i. Kila mjane atatakiwa kujisajili na kuorodhesha taarifa zake binafsi za msingi (Majina yake, Umri wake n.k) kwenye 'Daftari Maalumu' la Mtaa/kijiji husika na baadae taarifa hizi kuwasilishwa ofisi ya Kata ili ziweze kuunganishwa na kuwasilishwa katika ngazi ya Halmashauri, Mkoa na Taifa.

ii. Kutakuwepo na zana muhimu ya kumuwezesha mjane kutoa taarifa za hali yake kifamilia na wategemezi, ambapo kila mjane atatakiwa kutoa taarifa za hali ya familia ikiwa ni pamoja na idadi ya watoto, umri na hali zao Mfano:- Wanaosoma ni wangapi, walio vyuo vikuu na walio makazini n.k.

iii. Kila mjane aliyefungua Shauri la Mirathi atatakiwa kutoa taarifa za Mirathi na mwenendo wa ushughulikiaji wa mirathi hiyo.

iv. Kila Mjane atatakiwa kueleza changamoto anazokumbana nazo kama mjane ziwe za mila na desturi au zozote zile ili mradi zinakwamisha ustawi wa familia ili zifahamike na kutafutia utatuzi wa haraka katika ngazi husika. .

v. Kila mjane atashauriwa kujiunga kwenye vikundi vya wanawake au kuunda vikundi vya wajane kama idadi inatosheleza kwenye Mtaa/kijiji husika ili iwe rahisi kupata huduma za kiuchumi na kijamii kama mwanamke.

vi. Wajane watahamasishwa kujiunga kwenye majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi kuanzia ngazi ya Mtaa/kijiji

husika hadi ngazi ya Taifa ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi.

vii. Taasisi, wadau wa wanawake/Wajane, vyama vya Wajane Tanzania na Asasi za Kiraia zinazotoa huduma kwa wajane zitatakiwa kutumia takwimu zilizopo kwenye Halmashauri husika kupitia ofisi za Kata na Mtaa/kijiji husika ili huduma zinazotolewa zijulikane katika Mamlaka husika. viii. Wasaidizi wa Kisheria wana wajibu wa kushiriki kutoa elimu na kutatua changamoto za wajane za Kisheria;

## 3.2 Shirikisho la Wajane

Katika kuimarisha uratibu wa kundi la Wajane, kutakuwa na shirikisho la wajane ambalo litahusika kuratibu vyama vya wajane vilivyopo nchini. Shirikisho hilo litaundwa kwa kuzingatia taratibu za uanzishaji chombo kama hicho nchini. Kujiunga kwenye shirikisho itakua ni hiyari ya chama husika. Jukumu la shirikisho itakuwa kuunganisha vyama vya wajane kwa maendeleo ya wajane hapa nchini.

## 3.3 Uteuzi wa Mratibu wa Wajane

Kila ngazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekretariati za Mikoa na Wizara yenye dhamana na masuala ya Wanawake itateua mratibu atakayehusika kushughulikia masuala ya wajane. Mkuu wa Taasisi /Mamlaka husika atateua mratibu (mratibu anapaswa kuwa mtaalam wa Maendeleo ya Jamii kama hayupo mtaalam mwingine

aliyopo katika maeneo hayo atateuliwa ili kutekeleza jukumu hilo la uratibu.

### 3.4 Majukumu ya Mratibu

Masuala ya wajane katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yataratibiwa chini ya dawati la uwezeshaji wananchi kiuchumi na kupunguza umaskini. Mratibu wa wajane aliyeteuliwa katika ngazi husika atatakiwa kuhakikisha anashughulikia yafuatayo katika kuratibu kundi hili:-

i. Kutambua na kutunza orodha ya wajane ikiwa pamoja na kuhakikisha anatambua changamoto zao na mikakati ya ufumbuzi kwa kushirikisha wadau wengine.
ii. Kusimamia na kuhakikisha orodha ya wajane inahuishwa kwa kila robo na kufanya tathimini ya huduma zinazotolewa kwa wajane na wadau kama zinakidhi kutatua changamoto.
iii. Kuratibu vikao vya robo mwaka vya wadau kwa ajili ya kujadili masuala yanayohusiana na Wajane katika ngazi zote.
iv. Kuwa kiungo baina ya Serikali na Wadau ikiwemo Chama/Umoja wa wajane katika kuhakikisha kuna utekelezaji unaozingatia Sheria, Sera, taratibu na kanuni za Nchi katika kuhudumia wajane

## SURA YA NNE: MAJUKUMU YA WADAU

### 4.1 Wajibu na Majukumu ya Wadau

Mwongozo huu utatekelezwa sambamba na Mipango, Sheria, Sera, Mikakati na Programu nyingine za Kitaifa zinazojielekeza katika kuhudumia wanawake na kundi la wajane nchini. Majukumu ya Wadau muhimu wanaohusika na uratibu, usimamizi na uendeshaji wa Kundi la Wajane yameainishwa ili kutoa urahisi wa utekelezaji. Wadau hao ni OR-TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya Katiba na Sheria, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi, Wajane, Viongozi wa Dini, na Wadau wa maendeleo.

### 4.2 Ofisi ya Waziri Mkuu

Ofisi hii itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Uratibu wa Kundi la Wajane kupitia Baraza la uwezeshaji wananchi Kiuchumi.

ii. Kutoa Miongozo na maelekezo kwenye Wizara za Kisekta kuhusiana na Kundi la Wajane kama mojawapo ya makundi yanayotakiwa kupewa kipaumbele kwenye Mfuko wa uwezeshaji wananchi Kiuchumi na majanga/maafa kwa wajane.

iii. Utafutaji wa Rasilimali kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Kundi la Wajane.

Kutoa Miongozo na maelekezo kwenye Wizara za Kisekta na wadau wanaojishughulisha na masuala ya wajane wenye ulemavu

nchini; iv. Uratibu wa Kundi la wajane wenye Ulemavu kuhusiana na fursa za kijamii kiuchumi, kiasiasa na kisheria;

### 4.3 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Wizara hii ina dhamana ya kuratibu kundi hili na itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kutoa maelekezo ya kisera, kisheria na miongozo kuhusu uratibu wa wajane;
ii. Kuandaa na kuhuisha Mwongozo wa Uratibu na uendeshaji wa kundi la wajane;
iii. Kuratibu utoaji wa mafunzo kwa waratibu wa kundi la Wajane katika ngazi ya Kitaifa, Mikoa na Serikali za mitaa;
iv. Kubuni mikakati mbalimbali ya kuwainua Wajane kiuchumi kwa lengo la matokeo endelevu;
v. Kuratibu utekelezaji wa mwongozo wa Wajane kwa kushirikiana na TAMISEMI;
vi. Kuratibu ushiriki wa wadau na hasa Asasi za Kiraia katika kuhakikisha Wajane wanapata haki zao za msingi;
vii. Kuratibu uendeshaji wa Kundi la Wanawake Wajane na kujenga uwezo wa viongozi wa Kundi la Wajane katika ngazi zote.
viii. Kutoa elimu za uwezeshaji na uhamasishaji wa shughuli za kiuchumi kwa Kundi la Wajane.
ix. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Kundi la Wajane kwa kushirikiana na wizara za kisekta.Kujenga uelewa

Kwa jamii kuhusu Kundi la Wajane na namna ya kulipa kipaumbele.

x. Kupokea taarifa ya kila robo mwaka kutoka - TAMISEMI xi. Utafutaji wa Rasilimali kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Kundi la Wajane.

xii. Kuwaunganisha wajane na fursa za kiuchumi ikiwa ni pamoja na mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inayotoa mikopo yenye masharti na riba nafuu xiii. Kuratibu uteuzi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii kuwa Waratibu wa Kundi la Wajane ngazi zote.

xiv. Kufanya ushawishi wa kurekebisha na/au kutungwa kwa Sheria zitakazoondoa mila na desturi kandamizi kwa wajane.

## 4.4 Ofisi ya Rais TAMISEMI

Ofisi ya Rais - TAMISEMI itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia uratibu na uendeshaji wa Kundi la Wanawake Wajane katika ngazi ya Mikoa na mamlaka ya Serikali za Mitaa.

ii. Kutoa maelekezo ya uteuzi wa Afisa Maendeleo ya Jamii kuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za Kundi la Wajane katika ngazi za Mkoa, Halmashauri na Kata iii. Kuratibu upatikanaji wa taarifa za robo mwaka kutoka tawala za mikoa, kupokea, kuchambua na kuandaa taarifa ya pamoja na kuiwasilisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;

iv. Kusimamia utengaji wa bajeti, uratibu, uendeshaji na utekelezaji wa majukumu ya Kundi la Wanawake Wajane katika ngazi za

Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Kuweka Kasma ya utekelezaji wa Kundi la Wanawake Wajane).

v. Kuratibu na kuwaunganisha wadau wa maendeleo na Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kufanikisha uratibu na utekelezaji wa shughuli za Kundi la Wajane.

vi. Kujenga uelewa kwa jamii kuhusu Kundi la Wanawake Wajane na vipaumbele wanavyotakiwa kupewa katika maeneo yao kama kundi linalotakiwa kupata huduma za msingi ili kuondokana na umaskini.

vii. Utafutaji wa Rasilimali kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Kundi la Wajane.

viii. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi kwa kuhakikisha asilimia 30 za manunuzi zinatengwa kwa makundi maalum na kuwanufaisha wanawake
wakiwemo wajane.

ix. Kuhakikisha wajane wananufaika na fursa za mikopo nafuu ikiwemo ile yasilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

x. Kuwajengea uwezo waratibu wa wajane katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji.

## 4.5 Wizara ya Fedha

Wizara hii itakuwa na majukumu yafutayo:

i. Kuandaa na kutoa miongozo ya Mipango na Bajeti kwa Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uwezeshaji wa Kundi la Wajane.
ii. Kusimamia na kuratibu uwekaji wa kasma (vote) ya kuratibu kundi la wajane kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
iii. Kusimamia utekelezaji wa Miongozo ya Mipango na Bajeti.
iv. Kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Kundi la Wajane

## 4.6 Wizara ya Katiba na Sheria

i. Kuratibu utoaji wa elimu kuhusu masuala ya kisheria kwa kundi la Wajane katika ngazi zote kwa kushirikiana na Wasaidizi wa Kisheria.
ii. Kuhakikisha wajane kama ilivyo kwa makundi mengine katika jamii wanapata uelewa kuhusu Sheria na haki zao
iii. Kufanya mapitio ya sheria ambazo ni vikwazo kwa maendeleo ya wajane.

### 4.7 Tawala za Mikoa

Sekretariati za Mikoa zitakuwa na Majukumu yafuatayo:-

i. Kuteua Afisa Maendeleo ya Jamii atakayeratibu na kusimamia shughuli za Kundi la Wajane katika ngazi ya Mkoa;
ii. Kusimamia uratibu na uendeshaji wa Kundi la Wajane katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri;
iii. Kuratibu uandaaji wa taarifa za robo mwaka za utendaji wa Kundi la Wajane katika ngazi ya Halmashauri, kuzichambua, kuandaa taarifa ya pamoja ya Mkoa na kuziwasilisha TAMISEMI;
iv. Kutenga bajeti kwa ajili ya uratibu na utekelezaji wa shughuli za Kundi la Wajane kwenye Mkoa;
v. Kuratibu ushiriki wa wadau na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya uendeshaji wa kundi la wajane;
vi. Kusambaza Mwongozo na kutoa elimu ya uratibu wa kundi la wajane katika ngazi za Halmashauri.

### 4.8 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka hizi kwa maana ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Miji Midogo na Majiji zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

i. Kuteua Afisa Maendeleo ya Jamii atakayeratibu na kusimamia shughuli za Kundi la Wajane katika ngazi ya Kata na Halmashauri;
ii. Kusimamia uratibu na uendeshaji wa Kundi la Wajane katika ngazi ya kata, mtaa/kijiji;
iii. Kusimamia mikutano ya Kundi la Wajane katika ngazi ya Halmashauri kila baada ya miezi sita katika mwaka wa fedha;
iv.

Kupokea taarifa za utendaji wa Kundi la Wajane katika ngazi ya Kata na Mtaa/Kijiji, kuzichambua, kuandaa taarifa ya pamoja na kuziwasilisha ngazi ya Mkoa;

v. Kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Kundi la Wanawake Wajane la Halmashauri na kuingizwa kwenye mpango wa bajeti – MTEF;

vi. Kuwaunganisha wanawake wajane na fursa za kiuchumi hasa mitaji, masoko, Majukwaa ya

uwezeshaji wanawake kiuchumi na mikopo ikiwa ni pamoja na ile inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri; vii. Kutafuta vyanzo vingine vya fedha za kuwezesha uendeshaji wa Kundi la Wajane;

viii. Kuwaunganisha wajane na taasisi, Asasi za kiraia ix. ,Watoa huduma wa msaada wa kisheria katika Halmashauri ili waweze kusaidia kutatua changamoto zinazowakumba na kupata msaada wa kisheria;

x. Kuratibu ushiriki wa wadau na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya wajane;

xi. Kuwatambua wasaidizi wa Kisheria na kuwaunganisha na wajane kwa ajili ya kutatua changamoto za kisheria zinazowakabili.

## 4.9 Ofisi ya Kata

Ofisi ya kata itakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:-

i. Kuratibu na kusimamia shughuli zote za Kundi la Wajane;

ii. Kupokea, kusimamia na kutekeleza miongozo mbali mbali ya majukumu ya Kundi la Wanawake Wajane kutoka ngazi ya Halmashauri; iii. Kusimamia uendeshaji wa Kundi la Wanawake Wajane katika ngazi ya kata, kuandaa taarifa ya pamoja na kuziwasilisha ngazi ya Halmashauri;

iv. Kubaini vipaumbele vya mahitaji ya Kundi la Wanawake Wajane na kuviwasilisha kwenye Halmashauri ili kutengewa bajeti ya utekelezaji wa shughuli za Kundi la Wajane;

v. Kuwaunganisha wajane na fursa za kiuchumi hasa mitaji, masoko, Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi la Mtaa/kijiji,Kata na mikopo ikiwa ni pamoja na ile inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri; vi. Kushirikiana na Wasaidizi wa Kisheria katika kutatua changamoto za kisheria za wajane kwa ajili ya kutatua changamoto za kisheria zinazowakabili;

vii. Kutafuta vyanzo vingine vya fedha za kuwezesha uendeshaji wa Kundi la Wajane.

**Tanbihi:** *Endapo Ofisi ya Kata haina Afisa Maendeleo ya Jamii majukumu hayo yatatekelezwa na Afisa Mtendaji kat*

### 4.10 Ofisi ya Mtaa/ Kijiji

Ofisi hii kupitia Afisa mtendaji wa Kijiji/Mtaa itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kupokea, kusimamia na kutekeleza miongozo mbali mbali ya majukumu ya kundi la Wajane kutoka ngazi ya Kata;

ii. Atawataka kwenda na cheti cha ndoa na cheti cha kifo iii. Kuitisha mikutano ya wananchi kwa ajili ya kuwajengea uelewa kuhusu dhana ya kundi la Wajane; iv. Kusimamia zoezi la uorodheshaji wa taarifa za Wajane waliopo kwenye Mtaa/kijiji husika na kuzihuisha kila robo kwa ajili ya kuwasilisha ofisi ya kata;

v. Uratibu na usimamizi wa kundi la Wajane katikangazi ya mtaa/kijiji ikiwa ni pamoja na kuanisha

vi. changamoto wanazokumbana nazo kama vile mila na desturi kandamizi; vii. Kusimamia uendeshaji wa kundi la Wajane katika ngazi ya

Mtaa/Kijiji; viii. Kupokea taarifa za utendaji kutoka kwa viongozi wa Wajane ngazi ya Mitaa/Viijiji, kuzichambua, kuandaa taarifa ya pamoja na kuziwasilisha ngazi ya kata; ix. Kubaini vipaumbele vya mahitaji ya kundi la Wajane na kuviwasilisha kwenye kata ili kutengewa bajeti ya utekelezaji wa shughuli za Wajane;

x. Kuwaunganisha wajane na fursa mbalimbali za kujikwamua kiuchumi. ;

xi. hhhhhh

## 4.11 Asasi za Kiraia

i. Kutoa elimu kuhusu haki na wajibu wa Wajane katika shuguli za kila siku.

ii. Kutoa msaada wa kisaikolojia na unasihi kwa wajane. iii. Kuwezesha wajane kwa fursa mbalimbali za kujikwamua kiuchumi

iv. Kutoa msaada wa kisheria kwa wajane.

v. Kuhudumia Watoto wa wajane kwa kuwapatia misaada ya kijamii kama vili elimu, afya, lishe n.k

## 4.12 Viongozi wa dini

i. Kuelimisha jamii juu ya haki na wajibu kwa wajane kwa kutumia nukuu za vitabu kulingana na jamii husika pasi kuathiri haki za kibinadamu/taratibu za kidini.

ii. Viongozi wa dini washiriki na wasimamie kikamilifu katika mirathi inayongoza sheria ya dini na vikao vya uteuzi wa usimamizi wa mirathi.

iii. Kuhamasisha juu ya kuimarisha upendo kwa wajane na jamii kwa ujumla.

iv. Kutoa msaada wa kisaikolojia na faraja kwa wajane.

v. Kuhamasisha wadau na jamii kwa ujumla kuwahudumia wajane.

### 4.13 Wajane

i. Kujitambulisha na kutoa taarifa binafsi za familia kwa viongozi wa Serikali ya mtaa/kijiji kama ilivyoainishwa katika kipengele namba i) Sura ya Tatu;
ii. Kutekeleza Mwongozo uliopo;
iii. Kushiriki mikutano inayoratibiwa katika eneo husika;
iv. Kushiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi na ngazi za maamuzi;
v. Kushiriki kutatua changamoto zao kwa kushirikiana na uongozi uliopo kwenye eneo husika.

**TANBIHI:** *Wizara zote licha ya majukumu yake kutotajwa moja kwa moja katika mwongozo huu, zitahusika na utekelezaji wa masuala ya Wajane yanayogusa sekta husika kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo.*

## SURA YA TANO: UFUATILIAJI NA TATHMINI

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum itaratibu kwa kushirikiana na OR- TAMISEMI na Wizara za Kisekta utekelezaji wa Mwongozo huu katika ngazi ya Taifa. Ufuatiliaji na tathmini wa Kundi la Wajane umejumuisha taratibu za uratibu na uendeshaji Kundi la Wajane ikiwa ni pamoja na upatikanaji na utoaji wa taarifa za wajane, usimamizi na utekelezaji. Sekretarieti itakuwa na wajibu wa kutoa miongozo na vigezo vya ubora wa taarifa, aina za taarifa, muda wa kutoa taarifa na mtiririko wa utoaji wa taarifa kwa Kundi la Wajane nchini.

## 5.1. Ufuatiliaji

Mamlaka husika kupitia mratibu wa kundi hili itakuwa na dhamana ya kufanya ufuatiliaji shirikishi wa utekelezaji wa shughuli za Kundi la Wajane kwa kufanya ufuatiliaji wa usahihi wa takwimu na utekelezaji wa Mwongozo huu. Upimaji wa utekelezaji wa Mwongozo huu utazingatia vigezo vikuu vifuatavyo:

i. Usahihi wa taarifa na uhuishwaji wa taarifa za
ii. wajane katika ngazi zote; iii. Utatuzi wa changamoto za wajane kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya wajane; iv. Uimarishaji wa Wajane katika ngazi zote ikiwa ni uundaji wa vikundi vya Wajane na kuwaunganisha na Majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi na fursa za mitaji na mikopo isiyo kuwa na riba na ile yenye riba nafuu;
v. Mafunzo ya kuwajengea uwezo Waratibu, wajumbe wa serikali za Mtaa/kijiji, wajasiriamali na wajane;
vi. Uzingatiaji wa utengaji na upatikanaji wa fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya Kundi la Wajane.
vii. Aina ya shughuli za kiuchumi na biashara zilizoanzishwa na vikundi vya wajane ikiwemo viwanda na ubunifu uliofanyika katika ngazi husika;
viii. Jumla mikopo iliyotolewa kutoka kwa mamlaka za serikali za mitaa, WDF, Taasisi za Fedha na wadau mbalimbali ikionyesha idadi ya wajane walionufaika;

ix. Mifumo na utaratibu iliyowekwa na Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutoa kipaumbele na shughuli za kundi la Wajane;

x. Shughuli zilizotekelezwa wakati wa maadhimisho ya siku ya Wajane Duniani na idadi ya Wajane waliofanikiwa katika kila Halmashauri; xi. Idadi ya maonesho ya biashara yaliyofanyika na Idadi ya wanawake wajane walioshiriki maonesho hayo;

xii. Takwimu za matukio ya kazi zilizotekelezwa na Kundi la Wajane katika ngazi mbalimbali, na xiii. Uwepo wa mifumo ya mawasiliano ya kundi la Wajane kuanzia ngazi ya Mtaa/kijiji hadi Taifa.

### 5.2. Tathmini

Tathmini ya uratibu na ufuatiliaji wa Kundi la Wajane italenga kuona kama Kundi hili limesaidia kubadilisha hali ya uchumi wa Mjane. Aidha, tathmini itaongeza wigo, ubora na ufanisi wa kundi hili na shughuli zilizofanyika. Hii itajumuisha huduma zinazotolewa na wadau wa kisekta. Tathmini hii itafanyika kila baada ya miaka mitatu kwa kuongozwa vigezo vya upimaji ufanisi vitakavyoandaliwa na itaangalia viashiria vifuatavyo:

i. Idadi ya Wajane waliotatuliwa changamoto za mirathi na uwezo wa Wajane kusimamia na kudai haki za msingi za familia ili kuondokana na umaskini;

ii. Idadi ya Vikundi vya Wajane vilivyoanzishwa na idadi ya vikundi na wajane waliojiunga kwenye Jukwaa la Uwezeshaji

Wanawake Kiuchumi; iii. Idadi ya Wajane waliopata mikopo ya asilimia 10, WDF, Taasisi za Fedha na fursa mbalimbali walizounganishwa nazo; iv. Idadi ya zabuni zilizotolewa kwa vikundi vya Wajane, kandarasi za Wajane kupitia wizara, Taasisi za Serikali kwa mwongozo wa PPRA 30% kutolewa kwa makundi maalumu wakiwemo wanawake (Wajane wakiwa wamojawapo);

v. Idadi ya viwanda vidogo na kati vya Wajane vilivyoanzishwa na ajira zilizotengenezwa;

vi. Shughuli ndogo ndogo za kiuchumi zilizoanzishwa; vii. Idadi ya Wajane waliowezeshwa kupata teknolojia rahisi na sahihi, na aina ya teknolojia za uzalishaji;

viii. Idadi ya shughuli za ujasiriamali za wajane zilizofanyika hususani biashara ndogo, kilimo, madini, usafirishaji, usindikaji, uhunzi n.k; ix. Idadi ya biashara ndogo zilizounganishwa na taasisi au huduma za kifedha (mikopo);

x. Idadi ya mikutano ya wajane iliyofanyika; xi. Mwitikio wa wajane katika mikutano iliyoandaliwa; xii. Idadi ya wajane walioshiriki matukio, mfano maonesho ya biashara na wakulima;

xiii. Idadi ya biashara za wajane zilizorasimishwa

## 6.0 HITIMISHO

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya kuimarisha uratibu na uendeshaji wa kundi la Wajane nchini kwa kuhakikisha Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia ,Wanawake na Makundi Maalum, OR– Tamisemi, Wizara za kisekta, Mamlaka za serikali za Mitaa, Taasisi, Asasi za Kiraia na wadau mbalimbali wanatoa kipaumbele kwa kundi la Wajane na watoto wao. Kuhakikisha wanapata huduma zote za msingi na kuondoa umaskini na aina zote za ukandamizaji dhidi ya Wajane ikiwemo za kimila na desturi, kiuchumi kama vile kupoteza haki za umiliki wa mali na kulazimishwa kurithiwa baada ya kufiwa na waume zao.

Mwongozo huu utasaidia kuwa na takwimu na taarifa za changamoto wanazokumbana nazo wajane nchini nzima, hivyo Wizara yenye dhamana na wajane kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau wataweza kutatua na kujibu hoja za wajane kwa wakati na kusaidia kuimarisha kaya na familia za wajane kuondokana na umaskini. Pia utasaidia kujenga ushirikiano katika utendaji na uratibu wa masuala ya Wajane baina ya Wizara yenye dhamana ya Wajane, TAMISEMI, Wizara za Kisekta, Baraza la Uwezeshaji wananchi kiuchumi, Taasisi za serikali, dini na binafsi, Asasi za Kiraia na wadau ili kwa pamoja kutoa kipaumbele kwa kundi la Wajane ili waweze kuchangia uchumi wa nchi kwa kushiriki kikamilifu katika kila nyanja na kuhakikisha wajane wenye

umri mdogo (child-widows)[1] pamoja na watoto wa wajane wanapata haki za msingi za afya na elimu.

Hivyo basi, Wizara inaamini Mwongozo huu utatumika kama nyenzo, dhana na dira muhimu katika kuratibu na kushughulikia masuala ya wajane na kuhakikisha Lengo kuu la Mwongozo huu ambalo ni Kuhakikisha muundo/mfumo wa uratibu, uendeshaji na usimamizi wa masuala ya kundi la Wajane unasimamiwa kikamilifu, pamoja na malengo yake mahususi yanafikiwa katika kiwango kilichokusudiwa.

## ORODHA YA MAANDIKO YALIYOTUMIKA


i. HelpAge International & Cordaid. 2021. A study of older people's livelihoods in Tanzania;

ii. Kirwen, M. C. 1979. African Widows: An Empirical Study of the Problems of Adapting Western Christian teachings on Marriage to the Leviratic Custom for the Care of Widows in Four Rural African Societies, (Mary Knoll, New York 10545). iii.

Mhoja M.E.M. 2008. Child-widows Silenced and Unheard: Human Rights Sufferers in Tanzania (London: Author House).

iv. Magoke-Mhoja, M.E. 2005. The Impact of Inheritance Customary law to the Status of Windows and Daughters in Tanzania: A Challenge to Human Rights Activists. In Bond, J (ed.) 'Voices of African Women' – (Durham North Carolina: Calorina Academic Press).

v. Mhoja, M. E. 1997. The Impact of Inheritance Customary Law on the Status of Widows and Daughters in Tanzania: A Challenge to Human Rights Activists, LL.M Dissertation, Georgetown University Law Centre.

vi. Mhoja, M. E 1995. Legal Status of Widows. In Friedrech Ebert Stiftung, (ed). Exposed to Social Insecurity Vulnerable Women and Girls in Tanzania, (Dar es Salaam: Amref). vii. Vlassoff 1990 viii. (Sheria ya ndoa, 1971) Ndoa - Ni muungano wa hiyari kati ya mwanamume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao yote.